kwa uvumilivu ule ule mtakatifu kujitoa kwa mapenzi ya Mungu ambao huonekana katika maisha ya Mitume wote. Akiongea juu Yake Mwenyewe alisema:

**"Uzuri wa kale amekubali kuwekwa katika minyororo ili kwamba binadamu aweze kuachiliwa kutoka katika kifungo chake, na amekubali kufanywa mfungwa ... ili ulimwengu wote uweze kuufikia uhuru wa kweli."**

## Mafundisho ya Baha'u'llah

Kiini cha mafundisho ya Baha'u'llah ni umoja - umoja wa Mungu, msingi mmoja kwa dini zote na umoja wa binadamu. Yeye husema:

**"Ninyi ni matunda ya mti mmoja na majani ya tawi moja."**

Baha'u'llah amefundisha kwamba kuna Mungu mmoja tu ambaye ndiye Baba na Muumba wa binadamu wote. Mungu amefanya dini kama njia ya mawasiliano na kumwelimisha mwanadamu kiroho na kuendeleza mbele ustaarabu wake. Baha'u'llah ameeleza kwamba matatizo ya ulimwengu wakati huu yatokana na kutokuwa na umoja. Mafundisho Yake yanatoa dawa ya matatizo haya - ile njia ielekeayo kwenye umojo na undugu ambao mwanadamu amekuwa analilia. Baadhi ya mafundishi ya Baha'u'llah ni kama ifuatavyo:

1. Kuna Mungu mmoja tu
2. Msingi wa dini zote ni mmoja
3. Dini lazima iwe chanzo cha umoja
4. Watu wote ni wa ukoo mmoja wa mwanadamu
5. Kila mtu lazima atafute ukweli yeye mwenyewe
6. Wanaume na wanawake ni sawa
7. Tabia ya aina yoyote ya kupenda au kuchukia bila sababu lazima iachwe.
8. Watu wote lazima waelimishwe
9. Watu wote lazima washughulikie amani ya ulimwengu
10. Lugha moja ya msaada kwa Ulimwengu
11. Upatano wa dini na sayansi
12. Jawabu la matatizo ya kiuchumi linahitaji utumiaji wa sheria za kiroho na za kimwili.

## Kazi ni Ibada

Kuna mafundisho mazuri mengi zaidi ambayo yameletwa na Baha'u'llah. Kati ya hayo ni kwamba katika wakati huu Mungu ameitukuza kazi ambayo inafanywa kwa nia ya kuhudumia binadamu kuwa ni ibada. Baha'u'llah hufundisha kwamba kazi ifanywayo kwa moyo mnyofu ni ibada, kwamba kila wazo, neno na kitendo kinachofanywa katika Utukufu wa Mungu na viumbe wake basi ni ibada. Itaonekana kwamba maisha yote ya mtu kama tutatekeleza fundisho hilo basi, yatakuwa ni sala moja kwa moja.

## Baadhi ya Maandiko ya Kibaha'i

**"Ee Mungu wangu! Ee Mungu wangu! Unganisha mioyo ya watumishi Wako na uwafunulie kusudi lako lililokuu. Wafuate amri Zako na kukaa katika sheria Yako. Uwasaidie, Ee Mungu, katika jitihada yao na uwape nguvu kukutumikia Wewe. Ee Mungu, usiwaache peke yao bali uongoze hatua zao kwa nuru ya maarifa Yako, na uzifurahishe roho zao kwa upendo Wako. Hakika, Wewe ndie Msaidizi na Bwana Wao."**


**"Enyi wanadamu! Hamjui kwa nini tuliwaumba ninyi wote kutokana na mavumbi yale yale? Ili asiweko yeyote wa kujitukuza juu ya mwingine. Fikirini wakati wote mioyoni mwenu jinsi mlivyoumbwa. Kwa kuwa tumewaumba ninyi nyote kutokana na kitu kile kile kimoja mnapaswa kuwa hata kama roho moja, kutembelea miguu ile ile, kula kwa mdomo ule ule na kuishi katika nchi moja . . ."**

**Kwa maelezo zaidi andika kwa:**

Baraza la Kiroho la Kitaifa la
Wabaha'i wa Tanzania
P.O. Box 585
Dar es Salaam
bahaitz@cats-net.com
http://www.bahai.org/worldwide-community/national-communities/tanzania/

**Swahili**

# Mungu Mmoja
# Dini Yake Moja


The Bahá'í House of Worship, Wilmette, U.S.A.

The Bahá'í House of Worship
100 Linden Ave., Wilmette, IL 60091
how@usbnc.org
www.bahaitemple.org
(847) 853-2300

The Bahá'í Faith
www.bahai.org
1-800-22UNITE

## Sala ya Umoja

**"Ewe Bwana mwema! Umewaumba wanadamu wote kutokana na wazazi wamoja, umekusudia kuwa wote wawe jamii ya nyumba moja, na mbele ya utakatifu Wako wote ni watumishi Wako, na wanadamu wamelindwa chini ya Hema Lako takatifu. Watoto Wako wamekusanyika kwenye meza Yako ya ukarimu na wameng'aa kwa ajili ya mwangaza wa neema Yako. Ee Mungu! Wewe u mwema kwa wote, umewajalia wote, umewalinda wote. Umewapa uzima wote, umemjalia kila mnyenyekevu uwezo wa akili na umewazamisha wanadamu wote katika bahari ya rehema Yako.**

**Ewe Bwana Mkarimu! Waunganishe watumishi wako katika kila nchi, acha dini mbalimbali zipatane, yafanye mataifa yawe taifa moja, ili wajione kama ukoo mmoja, wanadamu washirikiane kwa nia njema hasa na umoja.**

**Ee Mungu! Ikweze bendera ya Umoja wa wanadamu. Ee Mungu! Isimamishe Amani Kuu. Ee Mungu! Unganisha myoyo yetu iwe moyo mmoja. Ewe Bwana mwema! Tuburudishe kwa manukato ya upendo Wako; yachangamshe masikio yetu kwa sauti tamu ya Neno Lako, na utulinde katika kimbilio la Neema Yako.**

**Wewe u Mwenye uwezo, Mwenye nguvu; Wewe u msamehevu na Wewe ni Yule ambaye ana samehe makosa ya wanadamu."**

## Mungu Ni Mmoja

Binadamu tangu hapo mwanzo amekuwa na nia ya kumjua Muumba wake. Lakini kwa uwezo wake mwenyewe binadamu hawezi kumjua Yule ambaye hana mwanzo wala mwisho. Njia pekee ya kupata fununu ya Huyo ambaye hakuumbwa ni kwa kupitia Wadhihirishaji Wake Mwenyewe ambao wametokea kila baada ya miaka elfu moja kwa wastani.

Kwa jinsi hiyo wametokea Krishna, Abraham, Zoroaster, Musa, Buda, Yesu, Muhammad, na kwa wakati huu Bab na Baha'u'llah.

## Ufunuo Uendeleao

Ulimwengu unaweza kulinganishwa na shule ambapo kila daraja la maendeleo linahitaji mafundisho yaliyoendelea kulingana na kiwango cha binadamu ambaye daima anasonga mbele. Mafunzo yanayotelewa katika daraja au darasa moja hayafuti yale yaliyotolewa kwenye daraja lililopita bali yanaendeleza mbele elimu. Jambo hilo linaonekana vilevile kwenye dini, wakati dini moja inatokea baada ya nyingine. Baha'u'llah alisema,

**"Hizi kanuni na sheria, hizi taratibu zilizo imara, zimetoka kutoka chanzo kimoja, na ni mionzi ya Mwanga mmoja. Kwamba zinatofautiana moja hadi nyingine ihesabiwe kuwa ni kwa sababu ya matakwa ya nyakati mbali mbali ambamo zilitangazwa."**

Hii njia iliyotolewa na Mungu ijulikanayo kama "Ufunuo uendeleao" inaweza vile vile kulinganishwa na kuota (kukua) kwa mti: "Ua haliharibu tumba na wala tunda kuharibu ua; ni hatua mbali mbali za kukua kwa mti huo" Au ni kama kukua kwa mwandamu,

"Je, mtoto hajitoi kuwa kijana kuwa mtu mzima, lakini bado si mtoto wala kijana haangamii?"

Kwa hiyo kufuatana na maelezo hapo juu inaweza kusemwa kwamba Ufunuo wa Baha'u'llah, ambao ni wa kipekee katika ukamilifu wake, na kwa mataifa yote, na ikiwa unalingana na matakwa ya wakati huu, ni mfululizo wa Ufunuo Mtakatifu wa Wadhihirishaji wa Mungu waliopita.

## Baha'u'llah

Dini zote kuu zilizotokea ulimwenguni zinangojea kuja kwa Mwalimu mkuu, Mkombozi, ambaye ,wakati utakapowadia ataunganisha mataifa yote na kusimamisha utawala wa haki na amani. Jina la Mwalimu mkuu huyu linabadilika kutoka dini hadi dini. Kwa Wakristo ni kurudi kwa Roho ya Kristo; kwa Waislamu wa dhehebu la Sunni, kushuka kwa Roho ya Mungu (Yesu Kristo) na kwa Waislamu wa dhehebu la Shi'ih, kurudi kwa Imam Husayn; kwa wa Budha, Budha wa tano; kwa Wayahudi; Bwana wa Majeshi. Kila mmoja wa Waahidiwa hawa atatimiza jambo hilo hilo, kuleta pamoja dini zote, makabila na mataifa ya ulimwengu katika udugu na upendo.

Katika mwaka 1844 huko Uajemi, kijana mmoja, ambaye baadaye alichukua jina la Bab, yaani 'Lango' alitangaza kwamba wakati ulikuwa umewadia ambapo yule Mwahidiwa wa nyakati zote, Mtume Mkuu wa Ulimwengu, atadhihirisha kwa wanadamu. Katika miaka 6 ya kufundisha kwake maelefu ya watu walimwamini. Ujumbe wake ulienea kutoka pembe moja hadi pembe nyingine ya Uajemi na kila mahali ilikutana na upinzani mkubwa kutoka kwa viongozi wa dini na serikali. Katika kipindi kifupi hicho zaidi ya wafuasi wake 20,000 waliuawa na wengine wengi kufungwa.

Haikuwa mpaka 1863, miaka 19 baada ya kujitangaza Bab, ambapo Baha'u'llah aliutangazia ulimwengu kwamba Yeye ndiye aliyekuwa Mwahidiwa ambaye kuja kwake kulitabiriwa katika vitabu vitakatifu vya dini zote kubwa. Kwa maneno ya kifalme kama yafuatayo alitangaza:

**"Wakati ulioamriwa kwa watu na jamii ya dunia sasa umewadia. Ahadi za Mungu, kama zilivyoandikwa katika maneno matakatifu, zote zimetimizwa."**

Kwa sababu ya mafundisho Yake ya upendo na umoja Baha'u'llah alinyang'anywa mali yote aliyokuuanayo na pamoja na ukoo wake na wengi wa wafuasi wake, walihukumiwa kipindi cha miaka 40 ya kifungo, kuhamishwa kutoka nchini alikozaliwa na kuteswa. Baha'u'llah aliyakubali maisha haya ya utwezo na mateso